OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME

SHULE YA SEKONDARI INCHUGU,
S.L.P 207,
TARIME-MARA.
12/12/2020.

KUMB.NA.ISS/JI/19
Mzazi /Mlezi wa _____
Shule ya msingi aliyotoka_____Tarime(V)

YAH:MAAGIZO YA SHULE YA SEKONDARI YA INCHUGU

WILAYA YA TARIME MKOA WA MARA

MWAKA2020

1. UTANGULIZI
   a. Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya ya sekondari Inchugu kidato cha kwanza mwaka 2021.
   b. Shule ya sekondari Inchugu ni ya kutwa na ni ya mchanganyiko (Wasichana na Wavulana). Shule ipo katika kijiji/eneo la Kitagasembe kata ya Gwitiryo wilaya ya Tarime.
   c. Ni matumaini yangu kuwa mwanao atatumia nafasi hii vizuri kujifunza kwa bidii ndani na nje ya darasa wakati wote awapo shuleni.
   d. Ni wajibu wako mzazi/mlezi kuhakikisha kuwa mwanao unampatia maadili,wosia na mahitaji muhimu ya kila siku kama vile malazi,chakula,mavazi,matibabu na mengineyo.Unatakiwa kufuatilia maendeleo ya mwanao mara kwa mara kupata taarifa ya maendeleo ya mwanao kitabia na kitaaluma kila muhula .
   e. Ikiwa mwanao atapanga chumba ,mzazi/mlezi utawajibika kumtembelea na kupata taarifa kwa mwenye nyumba aliyopanga

mwanao ili kupunguza uhuru, tabia ya utoro usio na msingi, mambo ya mapenzi,utumiaji wa madawa ya kulevya na unywaji wa pombe.

f. Shule itafunguliwa mnamo tarehe 11/1/2021.Hivyo mwanao anatakiwa kuripoti shule tarehe 11/1/2021.Ikiwa mwanafunzi hataripoti shuleni kufikia tarehe 02/02/2021 unaweza kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kumzuia mwanao kusoma kwa kuwa ***elimu ni ya bure*** kwa hivi sasa.

2. SARE ZA SHULE

a. Sare za shule kwa wasichana ni sketi mbili (2), moja yenye rangi ya damu ya mzee na ya pili rangi nyeusi zenye mishono linda box na ziwe ndefu zenye kufunika magoti. Mashati mawili rangi nyeupe yenye mikono mifupi yasiyobana mwili(modo) pamoja na tai(2) mbili nyeusi na damu ya mzee.
b. Sare ya shule kwa wavulana ni suruali nyeusi mbili(2) zenye malinda mawili na zilizopindwa chini kwa mtindo “turn up” na zisizobana mwili (modo). Mashati mawili (2) rangi nyeupe yenye mikono mifupi yasiyobana mwili
c. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa kwa Kamba kwa wasichana na wavulana.
d. Soksi nyeupe kwa wavulana kadhalika kwa wasichana .Soksi za wasichana ziwe ndefu (Stocking).
e. Sweta rangi ya damu ya mzee (maroon) kwa wasichana yenye shingo ya V.
f. Sweta rangi ya bluu (blue) kwa wavulana yenye shingo ya V.
g. Mkanda mweusi usio na mapambo wala picha kwa wavulana.
h. T-shirt ya rangi ya damu ya mzee kwa wasichana na wavulana.

MAAGIZO YA KUZINGATIA KATIKA UVAAJI NA USAFI WA MWANAFUNZI

- Wakati wote shati lazima liwe limechomekewa na vishikizo vya shati vifungwe.

- Hairuhusiwi mwanafunzi kutumia vipodozi (kama vile angel face, skin make ups, lip sticks, deep face,wanjan rangi ya kucha, hina n.k
- Hairuhusiwi kuvaa heleni , pete,bangili na mapambo aina yoyote.
- Nywele zikatwe ziwe fupi. Hairuhusiwi kunyoa mitindo kama vile kiduku, panki. Kupaka madawa kama vile Carl, Breach, Golden hair Wave n.k
- Hairuhusiwi kufuga ndevu wala kuvaa kofia ukiwa shuleni.

3. VIFAA VYA KUJIFUNZIA

Mwanafunzi anatakiwa kuja shuleni na vifaa vifuatavyo;

a. Madaftari makubwa (Counter books Quire 2 au 3) idadi ni kumi (10)

b. Vifaa vya hesabu, yaani bofa(mathematical set).

c. Dictionary (English-English).

d. Begi la kubebea madaftari/vitabu.

e. Mathematical Table (Four figure) kilichochapishwa na Macmillan.

VIFAA VINGINE NI;

i. Kivuli cha cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa.

ii. Mfagio mmoja (chelewa).

MUHIMU: Ni lazima mwanafunzi aje na vifaa bvilivyotajwa hapo juu.

4.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995.Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu, sayansi , tekinolojia na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya

rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa shule.

Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote wanafunzi wenzake na jamii nzima kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahusiano mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
3. Kushiriki kwa makini kufanya maandalizi ya jioni(preparation) ukiwa unakaa hostel au bweni shuleni.
4. Kuwahi katika shughuli zote unazotakiwa kufanya.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika mipaka hiyo.
6. Kufanya usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa kuvaa.
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
9. Kutunza mali ya umma.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi, uvutaji sigara na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, kuberi ,shisha, mirungi n.k.
4. Kupigana/kupiga.

5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma/shule.
6. Kudharau bendera ya taifa.
7. Kuoa au kuolewa.
8. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
9. Kutoa mimba au kusaidia kutoa mimba.
10. Kugoma ,kuchochea, kugoma na kuongoza kuvuruga AMANI na USALAMA wa watu.
11. Kukataa adhabu makusudi.
12. Kuwa na simu ya mkononi.
13. Utoro uliokithiri (Utoro sugu).

KARIBU SANA INCHUGU

…….

MKUU WA SHULE

SAMWEL MATESO NDABUKAKIYE

simu.0756023891

HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME
SHULE YA SEKONDARI INCHUGU S.L.P 207 TARIME MARA TANZANIA
FOMU YA UTII WA MWANAFUNZI ANAYEJIUNGA NA SHULE

1. Ahadi ya utii kwa mwanafunzi
   Mimi(mwanafunzi)……..wa kidato cha ……..mwaka 20……
   Nakiri kuwa nimesoma sharia zote za shule na kuzielewa.Nakubali kutii sharia na taratibu zote za shule kama zilivyoainishwa na kwamba adhabu kali itatolewa endapo nitaenda kinyume na sheria hizo.

   Sahihi ya mwanafunzi……..tarehe …….

2. Ahadi ya mzazi/mlezi kushirikiana na shule kuhakikisha mwanafunzi anatii sheria za shule.
   Mimi…….wa mtaa wa/kijiji cha……kitongoji cha……ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi……anayejiunga kidato cha kwanza mwaka 20…….katika shule ya sekondari Inchugu, nakiri kuwa nimezisoma sheria za shule zote na kuzielewa na kuwa nitakubaliana na maelekezo yote yatakayotolewa na shule.
   Ninaahaidi kuwa nipo tayari kutoa ushirikiano wa kutosha kwa ajili ya maendeleo ya shule na mwanafunzi.

   Jina la mzazi…… Simu……
   Sahihi…….. Tarehe……..

   Muhimu: Baada ya kujaza fomu hii irejeshwe shuleni wakati mwanafunzi anaripoti shuleni.

HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME
SHULE YA SEKONDARI INCHUGU S.L.P 207 TARIME MARA TANZANIA
FOMU KWA AJILI YA KUJUA AFYA YA MWANAFUNZI

Fomu hii ijazwe na Mganga wa Hospitali ya wilaya/kituo cha Afya kinachotambuliwa na serikali na siyo mganga wa zahanati(iletwe shuleni siku ya kuripoti).

Full name (student)……Age……

1. Blood count……Red and white……..
2. Stool Examination…….
3. Urine analysis……
4. Syphilisis and other S.T.D…….
5. TB and Leoprosy test…….
6. Eye test…….
7. Ear test……..
8. Chest test…….
9. Plano test(Girls)
10. Spleen……..

Addition Information e.g defects or impairments, infections, chronic or family disease(e.g Sickle cell) e.t.c

……
……
……
……